## Maswali

1. Mbona Elimeleki na Naomi walienda kuishi Moabu?
2. Nini ilifanyika kwa Elimeleki alipokuwa Moabu?
3. Majina ya wake wawili walioolewa kwa wana wa Naomi waliitwa nani?
4. Nini ilifanyika kwa wana wa Naomi walipokuwa Moabu?
5. Naomi aliamua kufanya nini?
6. Ruthu aliambia Naomi nini?
7. Ruthu alitafutia Naomi chakula namna gani?
8. Nani alikuwa mzuri kwa Ruthu?
9. Mbona jamaa aliyekuwa karibu alikataa kununua shamba la Elimeleki?
10. Nani alioa Ruthu? Jina la mwanao liliitwa nani?

## Majibu

1. Walienda kuishi Moabu kwa sababu ya njaa.
2. Elimeleki alikufia Moabu.
3. Majina ya wake wawili yalikuwa Orpa na Ruthu.
4. Wana wa Naomi walikufia Moabu.
5. Naomi aliamua kurudi na aishi Bethlehemu.
6. Ruthu alisema, “Nitaenda utakakoenda, na nitaishi utakakoishi. Watu wako watakuwa watu wangu. Nitaabudu Mungu wako.”
7. Ruthu aliokota shayiri iliyoangushwa na watu waliokuwa wakivuna.
8. Boazi alikuwa mzuri kwa Ruthu.
9. Hakutaka kuoa Ruthu, aliyekuwa Mmoabu.
10. Boazi alioa Ruthu. Mwana wao aliitwa Obedi.

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM

**Awamu ya 2    Mwaka wa 2**

# 54 Ruthu

### Kwa Biblia

Ruthu mlango wa 1 mpaka 4

### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu anafurahia watu wakiwa wazuri kwa wazee au kwa wasiojiweza


### Somo

Elimeleki na Naomi walikuwa Waisraeli. Walikuwa na wana wawili. Waliishi kwa mji wa Bethlehemu. Nchi yao ilikuwa na njaa. Kila mtu alikuwa na njaa. Elimeleki alisikia kwamba kuna chakula kwa nchi ya Moabu. Alienda kuishi huko na familia yake.

Elimeleki alikufia kwa nchi ya Moabu. Naomi aliishi huko na wanawe wawili. Wanawe walipokua wakubwa, walioa wake wa Moabu. Wale wake waliitwa Orpa na Ruthu. Baadaye hao wana wawili nao walikufa. Naomi aliachwa na wale wakweze Orpa na Ruthu katika nchi ya Moabu. Naomi alikuwa wa huzuni na upweke kule Moabu. Aliamua kurudi Bethlehemu na aishi kule.

Naomi alijua kurudi Bethlehemu ni mwendo mrefu na mgumu. Alijua kwamba itakuwa vigumu kwa Orpa na Ruthu kuenda kuishi katika nchi ya Israeli kwa watu wasiowajua. Naomi aliambia Orpa na Ruthu wabaki kwa nchi yao ya Moabu pamoja na marafiki zao.

Orpa alibaki Moabu. Lakini Ruthu alipenda Naomi. Ruthu aliamini Mungu. Ruthu hakutaka Naomi aende pekee yake. Alitaka aende asaidie Naomi. Alisema, “Usiniambie nikuaache. Nitaenda utakakoenda. Nitaishi utakakoishi. Watu wako watakuwa watu wangu na nitaabudu Mungu wako.”




Naomi na Ruthu walisafiri mpaka wakafika Bethlehemu. Walipofika Bethlehemu ilikuwa wakati wa kuvuna shayiri.

Naomi na Ruthu hawakukuwa na pesa. Hawakukuwa na chakula. Naomi aliambia Ruthu aende kwa shamba ya shayiri. Lazima afwate nyuma ya watu wanaovuna shayiri. Hao watu walipoangusha shayiri Ruthu aliokota.

Kwa siku nzima iliyofuata, Ruthu alikaa shambani akiokota. Aliokota shayiri kwa shamba la Boazi. Boazi alijua kwamba Ruthu alikuwa amekuja kutoka Moabu. Alijua kwamba alikuwa mzuri kwa Naomi. Boazi alitaka kusaidia Ruthu. Aliambia Ruthu kwamba anaweza kuokota chakula kutoka kwa shamba lake wakati wote wa kuvuna.

Ruthu alipopeleka chakula nyumbani aliambia Naomi vile Boazi alikuwa mzuri kwake. Naomi aliambia Ruthu kwamba Boazi ni mmoja wa watu wa jamaa yake. Ruthu aliokota kwa shamba la Boazi muda wote wa mavuno.



Nchi hiyo ilikuwa na desturi. Mtu akifa na hakukuwa na watoto wakurithi shamba lake, mtu mmoja wa jamaa aliyekuwa wa karibu angeoa mke wake. Mwana wa hao angerithi shamba lililokuwa la mtu aliyekufa. Huyo mwana angeendeleza jina la familia. Mme wa Ruthu alikuwa amekufa. Hakukuwa na watoto wa kurithi shamba la familia. Hakukuwa na watoto wa kuendeleza jina la Elimeleki. Naomi alitoa maoni kwa Ruthu kama angeuliza Boazi anunue shamba la Elimeleki na amuoe.

Ruthu alikuwa na tumaini kwamba Boazi atawasaidia kwa kumuoa. Boazi alikuwa amekuwa mzuri sana kwao wakati huo wote wa kuvuna. Boazi alijua kwamba Ruthu amekuwa mzuri kwa Naomi. Ruthu alikuwa na bidii ya kutafutia Naomi chakula. Boazi alipenda kumuoa Ruthu. Alipenda wapate mwana ili aendeleze jina la familia ya Elimeleki. Lakini Boazi aliambia Ruthu kwamba kuna mtu wa jamaa aliye karibu zaidi na Naomi kuliko yeye. Mtu huyo anatakiwa apewe nafasi ya kwanza kununua hilo shamba na kuoa Ruthu. Boazi aliahidi Ruthu kwamba atazungumza na huyo mtu.




Boazi alikutana na yule mtu kwa lango la mji. Shuguli zote zilikuwa zikifanyika pale langoni. Boazi aliuliza huyo mtu wa karibu, “Unataka kununua shamba la Elimeleki?”Huyo mtu alitaka kuongeza shamba lingine kwa hivyo alikubali. Lakini Boazi alimwabia, “Ukitaka kununua hilo shamba itakubidi umuoe Ruthu Mmoabu.”

Yule mtu alibadilisha mawazo yake na kusema, “Sitaki kuoa mke kutoka Moabu. Mtu mwingine anaweza kununua hilo shamba na kuoa huyo mwanamke. Kwa hivyo Boazi alikubali kununua hilo shamba na kuoa Ruthu. Yule mtu wa karibu na jamaa alitoa kiatu kimoja kama maagano nao. Hiyo ilikuwa desturi ingine ya wakati huo.

Boazi alioa Ruthu na kumlinda. Walipata mtoto wa kiume wakamuita Obedi . Naomi alifurahi kuwa na mjukuu. Alizaidia Ruthu kumlea Obedi.

Ruthu aliamini Mungu. Ruthu alikuwa mzuri kwa Naomi. Mungu alimlinda Ruthu. Alikuwa na mme wa kumjali. Alikuwa na mwana. Mwana wa Ruthu, Obedi, ni babu wa mfalme Daudi.